# MAELEKEZO YA VIKARAGOSI VYA NGAMIA

Kila siku ya VBS, Matukio ya Ngamia, kuna onyesho la vikaragosi liloandikwa kwako baina ya Kamelot na Kamelia. Wanafunzi watafurahia kujua ngamia hawa wakati wa VBS. Tunafurahia kukupa maelekezo na violezo ili kuunda vikaragosi hivi viwili. Uko huru kutumia nyenzo tofauti au kutafuta kutoka kwa chenye kinapatikana katika eneo lako kwa bei nafuu.

1. Tafuta vitu ambavyo utahitaji.
   - Makasi
   - Penseli (ya kutafuta kiolezo katika kitambaa)
   - Gundi (inayofanya kazi kwa haraka katika kitambaa: Silikoni au gundi moto)
   - Kijazio, mstari wa kitambaa cha firashi, mita 1/2
   - Kadibodi ( Ili kuimarisha kinywa)
   - Sindano ya kushona iliyo na shimo kubwa
   - Uzi usio mzito
   - Pomponi ndogo (mipira inayofanana na uyoga)
   - Mita 1 ya kitambaa kilicho na rangi ya ngamia
   - Kipande kidogo cha kitambaa cheusi (cheusi au hudhurungi kwa pua), na kingine chekundu (cha mdomo), na kwa hiari cha waridi cha masikio
2. Pakua ukurasa wa kiolezo ya PDF na uchapishe nakala mbili za ukurasa mkubwa kwa kutumia karatasi ya 11x17 au A3 (au uchapishe katika kurasa ndogo na kizishikanisha kwa utepe). Chapisha nakala ya ukarasa mdogo kwa kutumia karatasi ya ukubwa wa Barua au A4.
   - Kiolezo cha kichwa cha Ngamia
   - Kiolezo cha mdomo
   - Kiolezo cha pua
   - Kiolezo cha masikio

Nunua kitambaa kinachohitajika kwa ngamia. Tunapendekeza kitambaa kilicho na nyuzi ngumu, kwa sababu hakiraruki wala kukunjuka. Hata hivyo, unaweza kutumia kitambaa chochote cha bei nafuu utakachokipata katika eneo unaloishi. Tunapendekeza kitambaa kigumu au thabiti.

Kiasi cha kitambaa kilicho hapo chini ni makadirio tu, beba kiolezo hadi dukani ukienda kununua kitambaa ili kuhakikisha utanunua cha kutosha.

Rangi ya ngamia, hudhurungi nyepesi au rangi ya kijivu mita 1

Nyekundu mita 1/8


Hudhurungi au Nyeusi mita mita 1/8 (ndogo ikiwezekana)

Uzi: 1/4  bumba la hudhurungi ya nywele.


1/3 bumba la rangi tofauti , pomponi (mipira inayofanana na uyoga) za ukubwa wa 13mm

## KUUNDA KIKARAGOSI CHAKO


1. Kata kitambaa cha mwili na kinywa
   - Kata vipande viwili vya mwili
   - Kata kipande kimoja cha kinywa
2. Shona vipande vya kichwa pamoja ila wacha kinywa kimefunguka na pia upande wa chini ambapo mkono wako utaingia.
3. Shona vipande hivi viwili pamoja kwa kinywa cha juu huku ukiwacha kingo zilizonyooka kama zimefunguka. Fanya hivyo kwa upande wa chini wa mdomo. Shonelea kingo fupi zilizonyooka kwa kichwa katika sehemu ya upande iliyofunguka. Wacha kingo refu zilizowazi kwa ndani ya kinywa.



4. Ukiweka kitambaa upande wa nje ukiwa ndani, fungua vipande vya kinywa na kushikisha kitambaa chekunde cha mdomo katika uwazi. Kunja kinywa chekundu kwa nusu ili kupima ambapo pembe za kinywa zinafaa kuunganishwa ili kufunguka vinavyofaa. Kwa umakini shona kuzunguka kinywa chekundu, ukikibandika kichwani.




5. Geuza upande wa kichwa ulio nje uingie ndani ili mshono wote uwe ndani. Kata vipande vya kadibodi kwa ndani ya kinywa. Iwapo unatumia kadibodi iliyoimarishwa, jaribu kuweka kiolezo huku upana ukiwa haupo katika mistari iliyoimarishwa ambapo inaweza kukunjika virahisi. Ikate kwa nusu na kutia utepe kutoka juu hadi chini, ukiwacha mwanya wa sentimita 2.
6. Kata vipande viwili vya kijazio (kijazio cha mto) takriban urefu wa mdomo, ila vipana kutosha kukunja kuwa gogo, jaza upande wa juu na chini wa sehemu ya pua kwa kipande cha kijazio. Tumia ya kutosha ili kufanya pua kuwa thabiti. Mkono wako haufai kuguza vipande vya kadibodi unapoendesha kikaragosi. Rudia kwa kipande kingine kikubwa cha kijazio kwa kichwa, sukuma kwa nguvu hadi kwa uso na kichwa, huku ukiachilia kining'inie chini hadi kwa shingo. Mkono wako utakuwa hapo mbele ya shingo na upande wa kwanza wa mdomo huku ukiendesha kikaragosi.
7. Zungusha mita kadhaa za uzi juu ya mkono wako, huku ukinyoosha vidole vyako ili kuifanya kuwa rahisi kutoa. Funga katikati na kunyoosha vitanzi ili kuunda bumba la "nywele" na kuibandika juu ya kichwa kwa kutumia gundi ya Silikoni.
8. Iwapo kope zitatakikana (kama tulivyotumia na Kamelot) chora ruwaza za kuzunguka katika karatasi katika kitambaa kilicho na rangi ya ngamia na kuzikata. Kwanza, weka gundi katika uso, halafu bandika kope za macho juu kwa kutumia kidole chako kuinua sehemu ya katikati kiasi ndio zisishikane na kuwa bapa. Iwapo unaunda Kamelia, unaweza kutaka kubandika kope za macho ambazo zimenunuliwa au kukatwa kutoka kwa kitambaa cheusi.
9. Masikio yanaweza kuwa makubwa kwa kuchora ruwaza iliyotolewa au kuchongwa ili kuwa ndogo. Huku ukiingiza waridi kama tulivyofanya na Kamelia, pia ni kwa hiari. Tulibandika hemu kuzunguka sehemu ya nje ya sikio ili kulifanya kukaa limejaa na nguvu baada ya kubandika kitambaa cha waridi.
10. Juu ya kitambaa cha sikio kilicho na rangi ya ngamia. Amua mahali pa kubandika masikio kwa



kichwa na iwapo utayapenda yakiwa yamelala bapa au yameingizwa ndani huku umeyakunja kiasi. Gundi iliyo moto ni nzuri sana kwa kazi hii.

11. Pua la Kamelia kwa urahisi ni kukata kuzunguka ruwaza ya pua ndogo katika kitambaa cheusi na kubandika mbili katika uso wake. Pua la Kamelot liko na ngozi iliyoongezwa kwa kufunika “matundu ya pua” huku ukikunja chini ya hemu ndogo ili kulipa upana mrefu na pua kubwa kwa kikaragosi.



12. Lijamu na mapambo ya Kamelia zimetengenezwa kwa kushona sindano na uzi wa kurembesha na kushonelea pomponi juu yake, huku ukiwacha nafasi ndogo kati. Kining’inize kitambaa kinachovutia jinsi unavyotaka na kukibandika mahali kinachofaa. Hili pia linaweza kufanywa kwa utepe uliojikunjakunja kwa Kamelot. Shada hii ilitengenezwa kwa kuzungusha utepe uliojikunjakunja juu ya vidole vinne, na kisha kuitoa kwa kuitelezesha, na kufunga upande mwingine kwa kubingirisha na kufunga sana. Kata upande wa mwisho mwingine ili kuunda shada iliyo na rangi nyingi. Bandika kwa lijamu lake, iliyotengenezwa na utepe uliojikunjakunja unaolizunguka pua lake.
13. Burudika ukizungumza kwa sauti inayofaa sana kwa kikaragosi.